JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS - IKULU

Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania, (MKURABITA)

Warsha ya Pili ya Walengwa wa MKURABITA Itakayofanyika tarehe 15.02.2006 Jengo la NSSF – Waterfront, Dar es salaam

Mada Juu ya Matokeo ya Ripoti ya Tathmini Sekta isiyo Rasmi

Imetolewa na

Menejimenti ya MKURABITA
15.02.2006

15 Februari 2006

Lengo na Madhumuni ya MKURABITA

- **Lengo** la Mpango ni kuwawezesha walengwa ambao ni makundi ama watu binafsi wanaoendesha biashara ama kumiliki rasilimali katika mfumo usio rasmi, ili waweze kushiriki kikamilifu katika mfumo wa kisasa wa uchumi wa soko huria.

- **MKURABITA** ni mpango uliodhamiria kuwawezesha walengwa kuleta mabadiliko ya mfumo wa kumiliki mali na kufanya biashara katika sekta isiyo rasmi kwenda katika mfumo wa sekta rasmi ya uchumi wa kisheria.

Madhumuni Maalum ya MKURABITA

Madhumuni maalum ya MKURABITA ni haya yafuatayo;

- Kujenga mfumo mmoja wa kanuni za kumiliki mali na biashara utakaounganisha na kuboresha kanuni zinazotumiwa na makundi mbalimbali ya jamii nchini ili kuunda mfumo mmoja wa kitaifa wa umiliki mali na biashara.
- Kuimarisha umoja nchini kwa kuunganisha sekta isiyorasmi na sekta rasmi katika uchumi na hivyo kurahisisha kazi ya serikali katika kusimamia uchumi wa Taifa.
- Kuwezesha rasilimali za wanyonge zinazomilikiwa nje ya mfumo rasmi kusajiliwa na kutambuliwa rasmi katika mfumo mpya wa kisheria ili ziweze kutumika kupata mitaji.

Madhumuni maalum ya MKURABITA

- Kuwandaa viongozi wa jadi na vijiji pia kuweza kuyyapokea mabadiliko yatakayoingiza umiliki wa mali na biashara zao katika mfumo mmoja wa kitaifa ili waweze kunufaika na fursa zilizopo kwenye uchumi wa kisasa wa soko huria.

- Kuboresha utekelezaji wa sera kuu za kiuchumi na fedha maadam wadau wote wamo katika mfumo wa mmoja wa soko.

Hatua za utekelezaji
Hatua ya Kwanza: *Tathmini ya sekta isiyo rasmi*

Mpango huu unaanza kwa kufanya tathmini ya sekta isiyo rasmi ili kuweza kueleza maana uya sekta isiyo rasmi na kutambua;

- Ukubwa wake (makadirio ya wadau halisi)

- Thamani yake katika uchumi wa nchi

- Kanuni na taratibu za uendeshaji, na mahali shughuli zilipo.
- Vikwazo vinavyowazuia wahusika kuingia katika sekta rasmi au vivutio vinavyowafanya wapendelee kuwa katika sekta isiyo rasmi.

Tathmini ya sekta isiyo rasmi

- Mapungufu au vikwazo vya kisheria katika kumiliki mali na kufanya biashara.
- Kujenga ufahamu na kuendeleza miundombinu inayowezesha serikali kupata ushirikiano wa maboresho ya umilikishwaji wa rasilimali na biashara na uanzishwaji wa utawala bora wa kisheria, hivyo kuileta serikali karibu na wadau wake.

Tathmmini hii imekwishafanyika na ilichukua miezi 9 toka Novemba 2004 mpaka Julai 2005, na ripoti yake ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Benjamin W. Mkapa mwezi Oktoba 2005

Nini maana ya sekta isiyo rasmi?

MKURABITA inachukua maana pana sana ya sekta isiyo rasmi.

- Inajumuisha shughuli zote za kiuchumi zisizofuata taratibu na sheria zilizowekwa na serikali. Hii inajumuisha biashara zote zisizokuwa na leseni, rasilimali isiyohamishika (ardhi na majengo) yasiyokuwa na hati miliki inayotambuliwa kisheria, hujumuisha pia shughuli zote za biashara ambazo mmiliki wake hatofautishi mali za biashara na binafsi (za mmiliki wake). Kwa mfano unaweza kuwa na leseni ya biashara lakini kama hutofautishi mali za biashara na za binafsi biashara hiyo iko katika sekta isiyo rasmi.
- Biashara zisizokuwa na utunzaji wa kumbukumbu za mahesabu, wala mikataba ya ajira ya wafanyakazi wake pia siyo rasmi.

Maana ya sekta isiyo rasmi?

•Biashara isiyoweza kutoa fursa ya kupanua mtaji kwa kutoa hisa au kupata mikopo pia siyo rasmi.

•Biashara isiyoweza kutoa fursa ya dhima ya ukomo (limited liability) hutafsiriwa kama biashara isiyo rasmi

•Rasilimali isiyohamishika (majengo au ardhi) isiyoweza kutoa fursa ya kuitumia kupata mikopo au kama dhamana ya kupata mali nyingine pia siyo rasmi.

Maana ya sekta isiyo rasmi inatokana zaidi na kukosa fursa katika soko linalopanuka.

Mfano wa Biashara zisizokuwa rasmi

Mifano ya biashara katika sekta isiyo rasmi

Mifano ya biashara katika sekta isiyo rasmi



Mifano ya biashara katika sekta isiyo rasmi

Mifano ya mali za majengo zilizo katika sekta isiyo rasmi



Mifano ya mali za majengo zilizo katika sekta isiyo rasmi

Muhtasari wa Tathmini ya Sekta isiyo rasmi

- Kuna sheria mbili za umiliki ardhi Tanzania Bara nazo ni;

- **Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999** inayohusu ardhi ya mijini na ardhi ya vijijini ambayo si ya vijiji (general land) na
- **Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999** inayotawala ardhi ya vijiji.

- Sheria hizi humilikisha ardhi kwa kutoa haki ya kutumia (right of occupancy)-Hati za Ukaaji

- Haki hizi za kutumia hutolewa kwa muda maalum isipokuwa ile ya ardhi ya kijiji ambayo haionyeshi kikomo cha kutumia.

Muhtasari wa Tathmini ya Sekta isiyo rasmi

- Mapungufu yamebainika katika kanuni, miundo mbinu na teknolojia za kugawia ardhi kwa matumizi mbali mbali, kuandaa mipango miji, kupima maeneo na viwanja, kutoa ardhi/kiwanja kwa waombaji, kuandaa na kutoa hati za ukaaji/utumiaji, kusajili hati hizo, kuratibu na kusimamia matumizi kama inavyoonyeshwa kwenye hati, kutathmini kwa ajili ya fidia inapobidi, kulipa fidia, kuidhinisha mabadiliko ya milki, kutumia ardhi na majengo kama rehani ili kupata mikopo na hata utambulisho rasmi wa mmiliki wa eneo husika
- Kwa ujumla umiliki na utumiaji wa ardhi kama nyenzo ya uchumi wa kisasa umegubikwa na urasimu na gharama kubwa.

Muhtasari wa Tathmini ya Sekta isiyo rasmi

- Tofauti na Tanzania bara, Zanzíbar ina mfumo mmoja wa umilikaji ardhi. Sheria za Ardhi ambazo zinatumika Zanzibar ni Sheria ya Umiliki Na. 12 ya 1992 (Land Tenure Act No. 12 of 1992) na Land Registration Act 1990. Kwa sheria hizi kama ilivyo kwa Tanzania bara ardhi yote ni mali ya Umma na husimamiwa na Serikali

- Sheria hizi za Ardhi hazijatekelezwa kwa ufanisi kwa kuwa vitengo vya utekelezaji havijaundwa kwa ukamilifu. Kwa mfano Masijala ya Ardhi, Bodi ya kusimamia milki ya Uhaulishaji wa Ardhi, na Bodi ya Upimaji wa ardhi. Kutokuwepo kwa Bodi ya upimaji Ardhi kunafanya upimaji wa ardhi kwa kutumia wapimaji binafsi usiwezekane kisheria.

Muhtasari wa Tathmini ya Sekta isiyo rasmi

- Serikali imefanya maboresho kwenye sheria za biashara zikiwemo sheria ya Makampuni, sheria ya ajira na sheria mpya katika maeneo hayo (Company Act 2002, Employment Act 2004) Hii ni hatua nzuri kuelekea urasimishaji. Hata hivyo kanuni zake hazijawa tayari hivyo utekelezaji haujaanza.

- Vilevile utafiti huu umebaini kuwa bado ni vigumu kwa mtu wa kawaida kuanzisha biashara, kuendelea kufanya biashara, na kuacha inapobidi ndani ya mfumo wa sheria zilizopo.

- Kuzingatia sheria na kanuni zote za biashara kumebainika kuwa ni kazi ngumu na yenye gharama kubwa.

Muhtasari wa Tathmini ya Sekta isiyo rasmi

- Kwa upande wa Tanzania Bara zipo sheria 77 ambazo zinawagusa wajasiriamali wa aina mbalimbali.

- Na zipo Wizara nane (8) zenye kutawala au kuongoza au kuratibu masuala ya biashara nchini na kila moja ikiwa na mfumo wake wa kisheria na kiutawala. Na taasisi za umma tano (5)

- Kwa upande wa Zanzibar Zipo sheria 63 zinazogusa shughuli za biashara.

- Zipo Wizara 9 zinazohusika na shughuli za biashara na taasisi za umma 3 zenye mamlaka na majukumu juu ya biashara.

MIUNDO YA BIASHARA ILIYOPO TANZANIA BARA	NGAZI	HATUA	MUDA	GHARAMA US $
Taratibu za kusajili na kuendesha biashara binafsi	3	28	86	234
Taratibu za kusajili kampuni binafsi ya Duka la madawa (Mbeya)	9	95	376	2669
Taratibu za kusajili kampuni binafsi ya Duka la kubadilisha fedha za kigeni Dar es Salaam.	10	95	283	3916
Taratibu za kusajili kampuni binafsi ya Duka la kubadilisha fedha za kigeni Mbeya.	10	103	379	5506
Taratibu za kuanzisha na kusajili ushirika	3	16	137	1829
Taratibu za kusajili kampuni za umma Duka la kubadilisha fedha za kigeni Dar es Salaam.	14	117	341	6290
Taratibu za kushughulikia Wakurugenzi wa kampuni walioghushi au kosa la jinai	3	24	266	183
Taratibu za kubadilisha katiba ya kampuni	3	26	127	422
Taratibu za kupinga makisio ya kodi inayotakiwa kulipwa	3	76	378	1378
Taratibu za mufilisi	5	33	256	2639
Taratibu za kufunga kampuni	-	10	399	2753

MIUNDO YA BIASHARA ILIYOPO TANZANIA VISIWANI				
Taratibu za kusajili na kuendesha biashara binafsi (Stone town)	3	33	50	353
Taratibu za kusajili kampuni binafsi ya Duka la madawa (Stone town)	10	90	232	1590
Taratibu za kusajili kampuni binafsi ya Duka la madawa Chake chake	10	97	219	1490
Taratibu za kufunga kampuni	-	10	571	1498
Taratibu za kusajili na kuendesha biashara ya kampuni binafsi za "kazi za mikono" (Stone town)	9	84	218	3891
Taratibu za kupinga makisio ya kodi inayotakiwa kulipwa	3	79	500	2108
Taratibu za kutatua migororo ya kibiashara kati ya Wafanyabiashara	11	97	616	2336
Taratibu za kusimamia mikataba kwa sheria za kimila	3	16	114	51
Taratibu za kutatua na kutoa maamuzi ya migogoro	2	13	67	656
Taratibu za manunuzi	4	22	199	2266
Taratibu za kupinga maamuzi ya kiutawala	3	15	570	1939

Muhtasari wa Tathmini ya Sekta isiyo rasmi

- Watanzania walio nje ya uchumi rasmi (wanafanya shughuli zao bila kuzingatia matakwa ya sheria kikamilifu) wamejiundia mfumo wa kijamii (kanuni na taasisi za kutekeleza shughuli zao).

- Kanuni hizo zina ubora wa kutosha kuwa msingi wa maboresho yanayokusudiwa na zimekuwa kama mbegu inayopandwa kelekea kuwa rasmi.

Mfumo wa kijamii wa kuendesha biashara na umiliki mali (ardhi na maiengo)

Mfano wa Mkataba wa Biashara ya ubia unaotamb ulika kijamii na si kisheria



Mfumo wa kijamii wa kuendesha biashara na umiliki mali (ardhi na majengo)

Utambulisho wa Mwenyejiti wa kitongoji Kibaha-kama njia ya kumtambulisha apewe mkopo benki



Mfumo wa kijamii wa kuendesha biashara na umiliki mali (ardhi na majengo)



Uuzaji wa Shamba Mkataba unaonyesh a mipaka kwa ramani



Mfumo wa kijamii wa kuendesha biashara na umiliki mali (ardhi na majengo)

Makubaliano ya kukopeshana Fedha Taslimu kwa dhamana (Rehani) ya Nyumba. Riba, Ushahidi, na dhamana ni vitu muhimu hata katika mikataba ya kisheria



MAKUBALIANO YA KUKOPESHANA FEDHA

SHILINGI MILIONI MOJA NA LAKI TANO

Leo Tarehe 8/5/2003 Mimi Peter Ngalason nimechukuwa shilingi milioni moja na laki tano kwa ndugu Michael Shirima kwa ajili ya kufanyia biashara.

Makubaliano yenyewe ni kwamba wakati wa kurudisha fedha itakuwa kurudisha na riba ya shilingi laki mbili (200,000/=) yaani shilingi milioni moja na laki Saba (1700,000/=) kwa mwezi wa mwezi mmoja.

Ikiwa mimi [illegible] nayo riba itaendelea kuongezeka.

Nimepokea shilingi milioni moja na laki Tano nitakaporudisha kurudisha fedha hizo basi nyumba yangu ya room Tisa ya Udongo itachukuliwa na ndugu Michael Shirima.

Makubaliano haya yamefanyika mbele ya:

Sahihi — 1. Joel Pachanya — Baba

Sahihi — 2. Ndaula Saibulu — Mama mzazi wa Peter ngalason

Sahihi — 3. Peter Ngalason — Anayekopa

Sahihi — 4. Michael Shirima Anayekopesha

Sahihi — 5. Prosper Peter. Mtoto wa Peter Ngalason

4/

Ukubwa wa sekta isiyo rasmi

- Asilimia 98 ya biashara zote na asilimia 89 ya mali zote hususan za majengo na ardhi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ziko katika sekta isiyo rasmi.

- Thamani ya mali za biashara inakadiriwa kuwa dola za kimarekani bilioni 2.9 (kwa fedha ya Tanzania shilingi 2,900,000,000,000)

- Thamani ya mali za ardhi na majengo inakadiriwa kuwa dola za kimarekani bilioni 26.4 (kwa fedha ya Tanzania shilingi 26,400,000,000,0000)

- Jumla ya mali za biashara, ardhi na majengo ni dola za kimarekani bilioni 29.3 (kwa fedha ya Tanzania shilingi 29,300,000,000,000). Thamani hii ni sawa na 'mtaji mfu' kwa sababu mali hizi haziwezi kutumika kupatia mikopo na kupanua mtaji.

Asanteni Sana
Kwa kunisikiliza
!